**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 29 Mei, 2024**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2024/2025.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka 2024/2025.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

252. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Takwimu ziko vipi juu ya makosa mbali mbali yaliyoripotiwa kwa miaka ya hivi karibuni kwa matukio ya mauaji, ubakaji, ulawiti, wizi wa watoo, kunajisi na usafirishaji haramu wa binadamu.

**Wizara ya Afya:**

107. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali imeanzisha Bima ya Afya kupitia Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma bora za afya. Pamoja na lengo zuri la Serikali la kuwasaidia wananchi kwa kuwapatia huduma rahisi na bora kupitia mfuko huu, bado kumejitokeza changamoto nyingi zinazohitaji utatuzi wa haraka.

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba huduma za bima kupitia mfuko huu bado hazipatikani katika baadhi ya hospitali ndani ya Zanzibar.

(b) Je, ni kwa namna gani na maeneo yepi ZHSF inashirikiana na NHIF katika kuwahakikishia wananchi wanapata huduma za afya bora.

(c) Je, ni hatua gani imefikiwa katika utekelezaji wa kifungu 2 (1), (2), na (3) cha Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar Na. 1 ya 2023.

145. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa tafiti zinaonyesha kuwa kinywaji maarufu cha ‘Energy Drink’ ni hatari kwa afya za wanywaji. Na kwa kuwa ripoti nyingi za kitabibu zinaonyesha kuwepo kwa ongezeko kubwa la matatizo ya moyo yanayowapata watumiaji wa kinywaji hiki sambamba na vifo vinavyoweza kuepukika, hali inayoigharimu na kuiongezea mzigo mkubwa wa matibabu Serikali.

(a) Je, kwa kiwango gani Serikali inalifahamu tatizo hili.

(b) Je, Serikali imewahi kufanya tathmini yoyote ya kitabibu juu ya kinywaji hichi na madhara yake.

(c) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni muda muafaka wa kupiga marufuku uzalishaji na utumiaji wa kinywaji hichi kwa lengo la kupunguza madhara kwa wananchi wake.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

192. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika kampeni maarufu kuhusiana na upatikanaji wa miti hapa nchini, ni ile ya 'Kata Mti' 'Panda Mti' ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kutunza mazingira na kuihifadhi miti yenye manufaa mbali mbali kwa wananchi wetu.

(a) Je, Wizara imefanya tathmini yoyote ya kasi ya ukataji miti na upandaji miti nchini.

(b) Je, uwiano uko vipi wa kiwango cha kupanda miti na kukuwa kwa miti hiyo.

(c) Je, Wizara inasimamia vipi na kudhibiti ukataji ovyo wa miti hapa Zanzibar

207. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ni aina gani ya kilimo bora ambacho kinazingatia uhifadhi wa mazingira yetu kwa mustakbali wa kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

155. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika bajeti zilizopita, Serikali ilidhamiria kuzijenga gati za Mangapwani, Malindi, Mkoani, Wete na nyenginezo lakini hadi leo hii bado hazijajengwa.

(a) Je, ni tatizo gani lililopelekea ujenzi wa gati hizi kukwama hadi leo.

(b) Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

225. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kumekuwa na changamoto ya ukosefu wa takwimu sahihi za utalii wa ndani.

Je, ni jitihada gani Wizara inazichukua katika kuhakikisha kwamba tunapata takwimu sahihi za utalii wa ndani.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

22. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Je, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Taasisi ya 'Global Communities' wamefikia hatua gani katika juhudi zao za kulipatia ufumbuzi jambo la lishe katika skuli zetu za msingi na chekechea.

189. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

(a) Je, Wiara yako imewahi lini kufanya tathmini juu ya idadi ya maabara katika shule zetu sambamba na ubora wa vifaa vya maabara.

(b) Je, tathmnini hiyo iko vipi.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

40. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Naipongeza sana Serikali kwa kujenga tangi la maji liliopo Raha na kuchimba kisima katika eneo la Junguni Kijuki katika shehia ya Ukunjwi, lakini mpaka sasa kisima kipya cha Kijuki hakijaanza kusambaza maji na bado wananchi wa Fundo, Raha, Mvote Madaniwa, Utaani na Ukunjwi wanapata shida.

(a) Je, ni kwa nini kisima kipya cha Kijuki hakijaanza kutumika.

(b) Je, Serikali imechukuwa hatua gani ya kukabidhi tangi la maji la Raha ili maji yaweze kupatikana.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2024/2025.

### Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2024/2025.

**Zanzibar,**
**29 Mei, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**